ConsultLine ya
Elimu Maalum

Maelezo ya familia na watetezi wa watoto
walio na mahitaji maalum

800-879-2301
Watumiaji wa TTY: PA Relay 711

Msaada kwa Wazazi

Mfumo wa elimu maalum unaweza kukanganya, na wakati mwingine ukakulemea. Wakati hali mpya au kutoelewana kunapoibuka, huenda ikawa vigumu kubainisha haki zako ni gani na ni chaguo gani zinazopatikana kwako.

Ili kuwasaidia wazazi na maelezo kuhusu elimu maalum, ConsultLine ilianzishwa kama huduma isiyolipishwa kwa wazazi na watetezi wa watoto wenye ulemavu na watoto ambao wanafikiriwa kuwa na ulemavu.

Ikiwa una maswali au hoja kuhusu elimu maalum, elimu ya wenye vipaji, Sehemu ya 504, au haki zako kama mzazi wa mtoto mwenye mahitaji ya kipekee, wataalamu wa ConsultLine wanaweza kukusaidia.

Unaweza kuwasiliana na ConsultLine kwa kupiga simu kwa 800-879-2301 au 717-901-2146, au unaweza kuomba ConsultLine wakupigie simu kwa kujaza fomu ya maombi ya mtandaoni kwenye www.odr-pa.org/contact-consultline.

ConsultLine hutoa huduma ya moja kwa moja kwa Kiingereza na Kihispania, na inaweza kuwahudumia wapiga simu kwa lugha nyingine na msaada wa huduma ya ukalimani.

ConsultLine ilianzishwa ili kuwahudumia wazazi na watetezi wa watoto wenye ulemavu. Mashirika na mawakala ambao wanatoa msaada kwa familia ya watoto wenye ulemavu wanaweza pia kutumia ConsultLine. Wahudumu wa shule wenye maswali wanapaswa kuwasiliana na Shirika la Elimu Maalumu kwenye 717-783-6913.

ConsultLine ni…

Laini ya moja kwa moja ya mtaalamu ambaye:

- Atasikiliza hoja zako na kujadili chaguo kuhusu mahitaji ya mtoto wako
- Atajibu maswali na kufafanua maelezo kuhusu sheria husika za serikali na jimbo
- Atajadili chaguo za kutatua kutoelewana kuhusu mpango wa mtoto wako ikiwemo:

  - Mchakato wa malalamiko wa jimbo
  - Ulinzi wa utaratibu
  - Uwezekano mwingine usio rasmi wa kusuluhisha mizozo
- Kutambua mawakala na mashirika ambayo yanatoa aina nyingine za msaada
- Kutoa rasilimali za kukusaidia kujifunza mengi kuhusu elimu maalum na haki ya mtoto wako ya elimu ya bure na inayofaa ya umma

Wataalamu wa ConsultLine…

- Hawatendi kama mawakili
- Hawatoi ushauri wa kisheria

Kabla upige simu kuhusu wasiwasi wako unaohusiana na shule…

Zingatia kujaribu baadhi ya chaguo hizi:

- Wasiliana na mwalimu, mshauri, na/au mwalimu mkuu wa mtoto wako
- Jadili wasiwasi wako na mkurugenzi wa elimu maalum wa shule yako

Unapopigia simu ConsultLine…

Tafadhali acha maelezo yafuatayo. Hii itamruhusu mtaalamu wa ConsultLine kuwasiliana na wewe kwa wakati unaofaa.

- Jina lako
- Nambari ya simu ya nyumbani, biashara na/au ya mkononi
- Wakati unaofaa kati ya siku tatu zifuatazo za kazi (kati ya 8.00 a.m. na 4:00. p.m.) kwa mtaalamu wa ConsultLine kukupigia simu
- Ujumbe mfupi kuhusu hoja au swali lako

Rasilimali kwa Wazazi

Msaada wa Kiufundi na Utatuzi wa Mizozo

Pennsylvania Training and Technical Assistance Network (PaTTAN)

800-441-3215 Mashariki
800-360-7282 Harrisburg
800-446-5607 Pittsburgh
Tovuti: www.pattan.net

PaTTAN hutumika kama tawi la mafunzo na msaada wa kiufundi la Idara ya Elimu ya Pennsylvania, Shirika la Elimu Maalum. Washauri wa PaTTAN hufanya kazi kwa kushirikiana na vitengo vya kati ili kutoa huduma katika maeneo ya ukuzaji wa kitaaluma, msaada wa kiufundi, na usambazaji wa maelezo ili kuunga mkono wilaya za shule katika Pennsylvania. Tovuti ya PaTTAN inajumuisha Ukurasa wa Wazazi wa maelezo, machapisho, na viungo vya mashirika mengine.

Ofisi ya Kutatua Mizozo (ODR)

Simu: 800-222-3353
Watumiaji wa TTY: PA Relay 711
Barua pepe: odr@odr-pa.org
Faksi: 717-657-5983
Tovuti: www.odr-pa.org

ODR hupanga na kusimamia upatanisho wa elimu maalumu wa Pennsylvania na michakato ya kisheria. ODR hutoa rasilimali kwa wazazi na mashirika ya kielimu ili kutatua mizozo ya kielimu ya watoto yanayotolewa na mfumo wa uingiliaji kati mapema, wanafunzi wenye vipaji (au wanaofikiriwa kuwa na vipaji), na wanafunzi wenye ulemavu (au wanaofikiriwa kuwa na ulemavu).

Vituo vya Rasilimali vya Jamii na Wazazi

Hispanos Unidos para Niños Excepcionales (HUNE)

(Hispanics United for Exceptional Children)

Simu: 215-425-6203
Barua pepe: huneinc@aol.com
Faksi: 215-425-6204
Tovuti: www.huneinc.org

HUNE huwawezesha wazazi wa watoto wa kipekee kupata elimu ya bure na bora inayofaa kwa watoto wao. Wanatoa mipango ya mafunzo kuhusu hali zote za elimu na msaada, ikiwemo huduma za mpito. Hune hutoa huduma, lakini hazijakomea kwa, wazazi wa Kihispania katika American Street Empowerment Zone ya Philadelphia.

Mission Empower

Simu na Faksi: 814-825-0788
Barua pepe: advocate@missionempower.org
Nambari ya Simu Isiyolipishwa: 855-825-0788
Tovuti: www.missionempower.org

Madhumuni – Kupitia elimu, utetezi, uwezeshaji na kushiriki kwa wazazi tunanuia kuhakikisha ujumuishaji kamili wa vijana wenye ulemavu katika hali zote za maisha katika jamii yao.

Maono – Mission Empower ina maono ya jamii ambayo vijana wote wenye ulemavu wanatumia vipaji na talanta zao kufuata ndoto zao huku wakibadilisha jamii yao kuwa bora zaidi.

Mafunzo ya Wazazi na Kituo cha Maelezo

Kituo cha Elimu kwa Wazazi na Uongozi wa Utetezi (PEAL)

Simu: 412-281-4404
Nambari ya Simu Isiyolipishwa: 866-950-1040
TTY: 412-281-4409 Barua pepe: info@pealcenter.org
Faksi: 412-281-4408 Tovuti: www.pealcenter.org

Kituo cha PEAL ni shirika la wazazi wa watoto wenye ulemavu kilichojitolea kuwasaidia wazazi na wataalamu. Kituo cha PEAL kinatoa warsha, mafunzo, na maelezo kuhusu uingiliaji kati mapema, elimu maalum, na elimu jumuishi kwa maeneo ya magharibi na kati ya Pennsylvania. Washauri wa wazazi wanapatikana ili kusaidia familia na maelezo kuhusu mchakato wa elimu maalum na mikakati ya kutatua matatizo.

Idara ya Elimu ya Pennsylvania (PDE) haibagui katika mipango yake ya elimu, shughuli, au ajira, kwa misingi ya mbari, rangi, imani ya kidini, ukoo, uanachama wa chama cha wafanyakazi, umri, jinsia, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, asili ya kitaifa, hali ya UKIMWI au HIV, ulemavu, au kategoria nyingine yoyote inayolindwa na sheria. Tangazo la sera hii linalingana na Sheria ya Jimbo ikiwemo Sheria ya Mahusiano ya Binadamu ya Pennsylvania na pamoja na Sheria ya Serikali, ikiwemo Title VII ya Sheria ya Haki za Raia ya 1964, Title IX ya Marekebisho ya Elimu ya 1972, Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji wa Tabia ya 1973, Ubaguzi kwa msingi wa Umri katika Sheria ya Ajira ya 1967, na Sheria ya Wamerikani wenye Ulemavu ya 1990.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu chapisho hili, au kwa makala ya ziada, wasiliana na: ConsultLine, 6340 Flank Drive, Harrisburg, PA, 17112; 800-879-2301; Watumiaji wa TTY: PA Relay 711.

Watu wafuatao wamechaguliwa kushughulikia maswali yanayohusu sera za kutobagua:

Malalamiko kuhusu ubaguzi shuleni:

Mwakilishi wa Mahusiano ya Kibinadamu
Idara ya Usajili
Tume ya Mahusiano ya Kibinadamu ya Pennsylvania:
(Human Relations Representative
Intake Division
Pennsylvania Human Relations Commission):
www.phrc.state.pa.us
Ofisi ya Mkoa ya Harrisburg: Simu (717) 787-9780, Ujumbe Mfupi (717) 787-7279
Ofisi ya Mkoa ya Pittsburgh: Simu (412) 565-5395, Ujumbe Mfupi (412) 565-5711
Ofisi ya Mkoa ya Philadelphia: Simu (215) 560-2496, Ujumbe Mfupi (215) 560-3599

Malalamiko dhidi ya Idara ya Pennsylvania ya wafanyakazi wa Elimu:

Idara ya Elimu ya Pennsylvania
Mwakilishi wa Nafasi Sawa za Ajira
Ofisi ya Rasilimali Watu
(Pennsylvania Department of Education
Equal Employment Opportunity Representative
Bureau of Human Resources)
Ghorofa ya 11, 333 Market Street
Harrisburg, PA 17126-0333
Simu: (717) 787-4417
Faksi: (717) 783-9348, TTY ya Simu ya Ujumbe Mfupi: (717) 783-8445

Maelezo kuhusu marekebisho katika Idara ya Elimu ya watu wenye ulemavu:

Idara ya Elimu ya Pennsylvania
Mratibu wa Sheria ya Wamarekani Wenye Ulemavu
Ofisi ya Rasilimali Watu
(Pennsylvania Department of Education
Americans with Disabilities Act Coordinator
Bureau of Human Resources)
Ghorofa ya 11, 333 Market Street
Harrisburg, PA 17126-0333
Simu: (717) 787-4417
Faksi: (717) 783-9348, TTY ya Simu ya Ujumbe Mfupi: (717) 783-8445

Maswali ya jumla kuhusu sheria au masuala ya kielimu:

Idara ya Elimu ya Pennsylvania
Kitengo cha Huduma za Shule
Mkurugenzi
(Pennsylvania Department of Education
School Services Unit
Director)
Ghorofa ya 5, 333 Market Street
Harrisburg, PA 17126-0333
Simu: (717) 787-4860
Faksi: (717) 783-6802, TTY ya Simu ya Ujumbe Mfupi: (717) 783-8445

Commonwealth of Pennsylvania

Tom Wolf
Gavana

pennsylvania
DEPARTMENT OF EDUCATION

ODR

OFFICE FOR DISPUTE RESOLUTION
6340 Flank Drive
Harrisburg, PA 17112-2764

Tupigie simu . . .

(800) 222-3353
(717) 901-2145
Watumiaji wa TTY: PA Relay 711

Tutembelee kwenye Wavuti . . .

www.odr-pa.org

revised 6/20